



**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU MAAMUZI YA
SERIKALI KUFUATIA UCHAFUZI WA MAZINGIRA UNAOTOKANA NA
UVUJAJI WA BWAWA LA KUHIFADHIA TOPESUMU (TSF) KATIKA
MGODI WA DHAHABU WA NORTH MARA**



16 MEI, 2019

Uvujaji wa maji yenye kemikali yanayotoka kwenye bwawa la kuhifadhia topesumu (Tailings Storage Facility – TSF) ya mgodi wa dhahabu wa North Mara ulianza kulalamikiwa na wananchi wanaozunguka mgodi huo tangu mwaka 2009. Taarifa za uchafuzi huo zilipelekea kuundwa kwa timu mbalimbali za wataalam wa Serikali katika vipindi tofauti ili kubaini uhalisia wa uchafuzi huo kwenye mazingira ikiwa ni pamoja na kuripotwa kwa athari za kiafya kwa wakazi na mifugo.

Kwa nyakati tofauti, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) liliendelea kufanya utafiti wa kina kuhusu uchafuzi wa Mazingira unaotokana na utiririshaji wa maji yenye kemikali unaotoka katika bwawa la kuhifadhi topesumu la mgodi. Kama moja ya hatua za karibuni, mnamo Tarehe 9 Januari, 2019 mgodi ulipewa maagizo ya kuzuia utiririshaji wa maji yenye kemikali kutoka kwenye TSF mara moja, ikizingatiwa kwamba utiririshaji huo ulikuwa ukiendelea kutokea kwa muda mrefu bila kutatua tatizo hilo. Mgodi huo vilevile uliagizwa kuhakikisha TSF mpya inajengwa ndani ya miezi minane kuanzia Januari 9, 2019.

Aidha Serikali kupitia timu ya makatibu wakuu wa wizara za Ofisi ya Makamu wa Rais; Maji; Madini; Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, walijadiliana na uongozi wa mgodi juu ya uchafuzi huu wa mazingira na kukubaliana juu ya muda maalum wa kutatua tatizo hili ili kunusuru uharibifu zaidi wa mazingira na afya za wananchi na viumbe hai kwenye maeneo ya ndani na nje ya TSF hiyo. Pande zote zilikubaliana ya kwamba tarehe ya mwisho kutatua tatizo hilo iwe ni 30 Machi 2019.

Timu ya wataalam wa Serikali katika kipindi cha tarehe 29 hadi 31 Machi 2019 ilifanya ukaguzi wa TSF ili kuthibitisha utekelezaji wa makubaliano yaliyofikiwa kuhusu kudhibiti wa uvujaji wa maji hayo yenye kemikali na kubaini kwamba uchafuzi huo ulikuwa bado unaendelea.

Mnamo tarehe 30 Aprili, 2019, mwezi mmoja baadaye, Uongozi wa mgodi uliandikia barua serikali kuitaaruifu juu ya hatua mbalimbali zilizochukuliwa na mgodi kuhusu udhibiti wa uvujaji wa maji yenye kemikali kwenye mazingira na kukiri kwa barua yao wenyewe kwamba uvujaji bado ulikuwa ukiendelea. Ndipo Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mh. Januari Makamba (Mb) na Waziri wa Madini Mh. Dotto Mashaka Biteko (Mb), na Mkurugenzi Mkuu wa Baraza (NEMC) wakiambatana na timu ya

wataalam wa Serikali wakafanya ukaguzi wa maeneo ya TSF na kuthibitisha kwamba kweli uchafuzi huo wa mazingira ulikuwa ukiendelea.


Hivyo basi, mgodi wa dhahabu wa North Mara unabainika kufanya makosa yafuatayo:

1. Kuendelea kutiririsha maji yenye kemikali zenye sumu kwenye mazingira kwa muda mrefu licha ya maelekezo ya Serikali ya kudhibiti uchafuzi huo;
2. Kutotimizwa kwa matakwa ya Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 pamoja na Sheria mbalimbali za nchi;
3. Kutoa taarifa potofu ya utekelezaji wa maagizo ya Serikali kwa nyakati mbalimbali;
4. Kutokutii amri na maelekezo mbalimbali ya Serikali licha ya kupewa muda wa kutosha wa utekelezaji.

Mazingira kwa ujumla yameathirika sana kwa muda mrefu bila kupatikana suluhu ya tatizo hilo, ambalo ni wajibu wa mgodi kulitatua. Kutokana na ukubwa wa athari zilizotokea kwenye mazingira pamoja na afya kwenye jamii unaotokana na uchafuzi huo, Serikali kupitia Baraza linatoa maelekezo yafuatayo kwa mgodi wa North Mara, ambayo yanatolewa kupitia “Amri ya Kizuizi” (Protection Order) kama inavyoainishwa kwenye sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 na kanuni za Tatmini za Athari kwa Mazingira na Ukaguzi za 2005 na kama zilivyorekebisha mwaka 2018;

1. Kulipa faini ya shilingi bilioni tano na milioni mia sita (5.6 bilioni) ndani ya siku kumi na nne (14);
2. Kuchukua hatua za ziada kudhibiti uchafuzi unaoendelea wa uvujaji wa maji yenye kemikali kutoka kwenye bwawa la tope sumu (TSF) ndani ya wiki tatu kuanzia tarehe ya 16 May 2019.

Imetolewa leo tarehe 16 Mei 2019 na



Dkt. Mha. Samuel G. Mafwenga

Mkurugenzi Mkuu

BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA - NEMC